# SHERIA YA NDOA
# NA
# SHERIA ZA MIRATHI, TANZANIA



**EQUALITY FOR GROWTH (EfG)**
**S.L.P 10618**
**DAR-ES-SALAAM, TANZANIA**
**SIMU: +255 22 2863293**
**BARUA PEPE:equalityforgrowth@gmail.com**
**TOVUTI: www.equalityforgrowth.org**

**KIMETAYARISHWA NA:**
**Equality for Growth (EfG)**



**KIMEANDALIWA NA:**
**Jane Magigita**

**MHARIRI**
**Rabia Ramadhani**

**KIMEFADHILIWA NA:**
**DFID - AcT Accountability in Tanzania Prorgamme**
**Ubalozi wa Finland, Tanzania**

**ISBN: 978-9987-9538-3-7**



# Yaliyomo


SHUKRANI iv

SEHEMU YA 1: SHERIA YA NDOA TANZANIA 1

1.1 Utangulizi: 1

1.2 Maana na Aina za ndoa 1

1.3 Utaratibu wa ufungishaji ndoa 1

1.4 Mambo ya Kuzingatia kabla ya kufunga ndoa 2

1.5 Dhana ya Ndoa 2

1.6 Kugeuza ndoa 3

1.7 Pingamizi kuzuia kufungwa kwa ndoa 3

1.8 Utaratibu wa Kusajili Ndoa. 4

1.9 Umiliki wa Mali, Haki na Wajibu wa wanandoa. 4

1.10 Talaka na Kutengana 6

SEHEMU YA 2 SHERIA ZA MIRATHI TANZANIA 8

2.1 Utangulizi 8

2.2 Aina za Sheria za Mirathi Tanzania 8

2.3 Wosia 10

2.4 Utaratibu wa Kufungua Mirathi 11

2.5 Haki na Wajibu kisheria wa Msimamizi wa Mirathi 12

2.6 Mtitiriko katika kulipa madeni ya marehemu 12

2.7 Masuala Kumi (10) Umuhimu ya kujadiliwa kuhusu Mirathi: 13

## SHUKRANI

Awali ya yote, EfG inapenda kuwashukuru wote waliofanikisha kwa njia moja au nyingine kukamilika kwa chapisho hili ambalo linalenga kutoa elimu kwa jamii ya Watanzania wengi wenye uhitaji wa elimu ya sheria. Lengo kuu la EfG ni kuwafikia waliojiajiri au wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi walio na mahitaji muhimu ikiwemo kuwajengea uwezo wa elimu ya biashara, kuimarisha vikundi na elimu ya sheria. Ni matarajio yetu kuwa elimu juu ya sheria za ndoa na mirathi kama zilivyofafanuliwa katika kitabu hiki itasaidia kuimarisha mwenendo mzima wa shughuli zao za kiuchumi kwa kutoa elimu juu ya haki ya kupata, kumiliki, kutumia na kulinda mali. Uwezekano wa mtu kupoteza mali yake aliyochuma ni mkubwa iwapo hatajua haki yake juu ya mali hiyo lakini pia kutofahamu haki hiyo kunaweza kumfanya mtu huyo kukiuka haki za wengine. EfG inaamini ulinzi salama wa biashara na mali kutampa mtu uwezo wa kuendesha biashara yake kwa ufanisi na hivyo kuongeza tija.



# SEHEMU YA 1

## SHERIA YA NDOA TANZANIA

### 1.1 Utangulizi:

Masuala ya ndoa Tanzania yanasimamiwa na Sheria ya Ndoa Sura ya 29 kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002. Sheria hii pamoja na mambo mengine inafafanua maana ya ndoa, aina za ndoa, mambo ya muhimu ya kuzingatia kabla ya kufunga ndoa na kipindi cha kufunga ndoa, haki na wajibu wa wanandoa, dhana ya ndoa, talaka na mengineyo.

Kwa mwanamke mfanyabiashara ni muhimu kufahamu haki zipi zimeainishwa katika sheria hii na ambazo kwa njia moja au nyingine zinaweza kusaidia kukuza biashara. Kwa kutofahamu, mfanyabiashara anaweza kupoteza haki zake za msingi pale inapotokea ndoa kuvunjika au kifo cha mwanandoa mwenzie.

### 1.2 Maana na Aina za ndoa

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Ndoa, Sura Na. 29 ya sheria za Tanzania kimetoa maana ya neno ndoa kuwa ni Muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudia kudumu kwa maisha yao yote. Pia sheria inatambua kuwepo kwa aina mbili (2) za ndoa yaani Ndoa ya mke mmoja na Ndoa ya wake wengi.

### 1.3 Utaratibu wa ufungishaji ndoa

Sheria ya ndoa imeainisha utaratibu wa ufungishaji ndoa kuwa wa aina tatu;

- Ndoa za kiserikali: Hizi ni ndoa zinazofungwa bomani au kwa Mkuu wa Wilaya kwa kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.
- Ndoa za kidini: Ndoa zinazofungwa kwa kufuata taratibu zilizoainishwa na taasisi za dini husika kama kanisa au msikiti.
- Ndoa za kimila: Ndoa zinazofungwa kwa kufuata mila na desturi za kabila husika.

  Ni muhimu ieleweke kwamba mwanamke hataruhusiwa kufunga ndoa nyingine iwapo ndoa yake ya awali haijavunjwa kwa talaka ya mahakama.

  Aidha mwanaume aliye katika ndoa ya mke mmoja hataruhusiwa kuoa mke mwingine.

| **Kumbuka** |
|---|
| Ni muhimu na ni utaratibu wa kisheria kusajili ndoa.<br><br>Ni muhimu kuwa na cheti cha usajili wa ndoa kwani ni utambulisho na uthibitisho wa kuwepo ndoa halali. |



## 1.4 Mambo ya Kuzingatia kabla ya kufunga ndoa

- Kuwepo na muungano wa hiari kati ya mwanamke na mwanaume kabla ya kufunga ndoa hufanya ndoa kuwa halali. Kifungu cha 16 cha Sheria ya Ndoa (marekebisho ya mwaka 2002) vinazuia kuwepo kwa ulaghai au udanganyifu wa kati ya mwanamke na mwanaume wanaotarajia kufunga ndoa.
- Muungano huo uwe unakusudiwa kuwa wa kudumu.
- Anayetaka kufunga ndoa asiwe katika ndoa nyingine. Hii ni kwa wale waliokwisha kufunga ndoa ya mke mmoja au kama muumini wa dini ya kikristo na endapo ni muumini wa dini ya kiislamu basi hataruhusiwa kuoa zaidi ya wake wanne. Kusiwe na ndoa inayoendelea.
- Wafunga ndoa wasiwe watu walio na mahusiano ya karibu ya damu au kindugu 'maharimu'. Sheria ya ndoa inazuia mtu kuoa au kuolewa na mzazi wake, baba au mama wa kambo, mtoto au mjukuu, mtoto wa kufikia au kuasiliwa, kaka au dada, shangazi au baba wa mjomba wake. (Kifungu 14 cha Sheria ya Ndoa).
- Wafunga ndoa wawe wametimiza umri unaokubalika kisheria ambao ni miaka 18 . Chini ya umri huo iwapo tu kibali kimetolewa na wazazi kwa binti asiye chini ya miaka 15 na mahakama kwa asiye chini ya miaka 14. Mwanaume anaweza kuruhusiwa na mahakama kuoa akiwa chini ya miaka 18 lakini si chini ya miaka 14 kama ataonyesha kuelewa jukumu lake kama mtu mzima.
- Lazima ndoa inapofungwa wanaotarajia kufunga ndoa wawepo, Kutokuwepo kwa wafungaji ndoa ni kinyume na sheria. Kwa mazingira Fulani hata hivyo sheria inaruhusu ndoa kufungwa ikiwa mmoja wa wafunga ndoa hayupo lakini amewakilishwa na mtu ambaye alikuwepo wakati mfunga ndoa ambaye hayupo, alipotoa ridhaa yake ya kuoa au kuolewa.
- Pia mfugishaji ndoa lazima awe na leseni ya serikali inayompa mamlaka.a.
- Ndoa inapofungwa lazima ishuhudiwe na mashahidi wasiopungua wawili wenye umri usiopungua miaka 18.

## 1.5 Dhana ya Ndoa

Je mwanamke na mwanaume walioishi pamoja kwa kipindi fulani bila kufunga ndoa wanaweza kuhesabika kuwa wanandoa?

Sheria inatambua dhana ya kuwepo kwa ndoa kati ya mwanamke na mwanaume walioishi pamoja bila kufunga ndoa iwapo mambo yafuatayo yatatimizwa:

- Iwapo watu hao wawili wameishi kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo paa moja.
- Majirani wanaowazunguka wanawachukulia kuwa ni mke na mume.
- Hakuna ndoa inayoendelea kutokana na maisha yao ya awali.
- Wametimiza umri unaokubalika kisheria wa kuoa au kuolewa (umri wa18 au zaidi).

  Iwapo mambo hayo manne yametimizwa, mahakama inaweza kuthibitisha kuwepo kwa ndoa kati ya watu hao wawili.



| Kumbuka |
| --- |
| • Ni mahakama pekee yenye uwezo kisheria kuthibitisha kuwepo au kutokuwepo kwa dhana ya ndoa.<br>• Ni vigumu kuthibitisha kuwepo kwa dhana ya ndoa iwapo mmoja wa wanandoa amefariki dunia. Wanandoa wanaoishi bila ndoa wanashauriwa kuhalalisha ndoa yao ili kuwa katika mazingira mazuri ya kudai haki hasa pale mmoja wa wanandoa anapofariki. |

## 1.6 Kugeuza ndoa

Sheria ya Ndoa inaeleza kuwa ndoa ya mke mmoja itaweza kugeuzwa kuwa ya wake wengi iwapo tu wanandoa, mke na mume watakubaliana kwa tamko la maandishi juu ya hiari yao kubadili ndoa hiyo. Sheria hairuhusiwi kugeuza ndoa ya kikristo kuwa ya wake wengi.

Ndoa ya wake wengi inaweza kugeuzwa kuwa ya mke mmoja iwapo mume ana mke mmoja na wanandoa hao kwa hiari wamekubaliana kufanya hivyo kwa tamko la maandishi.

Kulingana na Sheria ya Ndoa tamko la maandishi ni lile litakalofanywa mbele ya Jaji, hakimu mkazi au hakimu wa wilaya na kusainiwa na wahusika wote akiwemo mshuhudiaji.

| Kumbuka |
| --- |
| Ni kosa la jinai kufunga/kufungisha ndoa iwapo mtu huyo ana ndoa ya mke mmoja inayoendelea. |

## 1.7 Pingamizi kuzuia kufungwa kwa ndoa

Mke/wake anaweza kutoa pingamizi dhidi ya ndoa inayotarajiwa kufungwa kwa afisa msajili iwapo:-

- Kuongeza mke kutasababisha ugumu wa maisha kwa mke/wake waliopo pamoja na watoto kutokana na uwezo mdogo alionao mume.
- Mke mtarajiwa ana tabia mbaya au ana ugonjwa wenye kudhuru au kuambukiza na hali hiyo itasababisha matatizo makubwa katika familia.

### Jinsi ya kuwasilisha pingamizi:-

- Pingamizi juu ya kufungwa kwa ndoa litawasilishwa katika Baraza la Usuluhishi wa Ndoa au Mahakama au kwa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini.
- Pingamizi litasikilizwa kwa kuhusisha wanandoa watarajiwa, mpingaji, mashahidi na mtu yeyote atakayehitajika.
- Ndoa haitafungwa mpaka pingamizi hilo litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi au kuondolewa na mpingaji.Uamuzi uliotolewa utawasilishwa kwa msajili aliyepokea pingamizi hilo.
- Pingamizi linaweza kukubalika au kukataliwa katika uamuzi utakaotolewa.



**Kumbuka**

Msajili wa ndoa aliyepokea pingamizi hataruhusiwa kufungusha au kushiriki kufungisha ndoa iliyowekewa pingamizi na atachukua hatua zote za kisheroa zilizo katika uwezo wake kuzuia kufungwa kwa ndoa hiyo hadi hapo pingamizi litapotolewa au kuondolewa.

## 1.8 Utaratibu wa Kusajili Ndoa.

Ndoa yeyote iliyofungwa lazima isajiliwe na wanandoa kupewa cheti cha ndoa mara tu baada ya kufunga ndoa.

Iwapo ndoa ilifungwa kimila na haikusajiliwa, wanandoa wanaweza kufanya usajili wa ndoa hiyo kwa kuwasilisha maombi kwa msajili wa wilaya, kadhi au afisa msajili yeyote:

- Mwombaji ataandaa taarifa ya uthibitisho wa kuwepo kwa ndoa hiyo.
- Atawasilisha maombi na uthibitisho huo kwa msajili wa wilaya na afisa msajili.
- Cheti cha ndoa kitatolewa baada ya afisa msajili kuridhika na uthibitisho uliotolewa.

**Kumbuka**

Uthibitisho wa kuwepo kwa ndoa unaweza kutolewa kwa barua ya utambulisho inayothibitisha kufungwa kwa ndoa husika iliyotolewa na taasis au chombo cha kidini au ushahidi wa majina ya mfungishaji,

Ni muhimu na ni utaratibu wa kisheria kusajili ndoa.

Ni muhimu kuwa na cheti za usajili wa ndoa kwani ni utambulisho na uthibitisho wa kuwepo ndoa halali.

## 1.9 Umiliki wa Mali, Haki na Wajibu wa wanandoa.

Sheria ya Ndoa imeainisha haki mbalimbali za wanandoa. Kimsingi mke ana haki sawa na mwanaume katika ndoa.

Baadhi ya haki zilizoainishwa ni pamoja na;

- Haki sawa kwa mwanamke katika kupata, kumiliki na kugawa mali yake. Haki hii ni kwa mali zote zinazohamishika na zisizohamishika.
- Mwanamke ana haki ya kuingia katika mikataba, kushtaki na anaweza kushtakiwa, na
- Mwanandoa ana haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa kipindi cha ndoa.

### Umiliki wa pamoja wa mali

Mwanandoa ana haki ya kumiliki mali binafsi na pia kumiliki mali kwa pamoja na mwanandoa mwenzake.

Mali iliyochumwa kwa nguvu au jasho la wanandoa wote itahesabika kuwa ni mali ya pamoja katika ndoa.



| **Muhimu** |
| --- |
| - Je biashara unayofanya ni biashara binafsi au ni ya pamoja na mwanandoa mwenzako?<br>- Kama unamiliki mali pamoja na mwanandoa mwenzako, je katika biashara hiyo una hisa kiasi gani?<br>- Je jina lako liko katika hati muhimu za biashara au mali kama hati ya usajili, umiliki, leseni ?<br>- Je unawezaje kuthibitisha mchango wako katika biashara hiyo? |

## Umiliki Binafsi wa Mali

Mali iliyo katika jina la mwanandoa mmojawapo itahesabika kuwa mali binafsi ya mwanandoa huyo. Dhana hii inaweza kukanushwa na mwanandoa mwingine kwa kuthibitisha vinginevyo. Mali iliyo na majina yote mawili ya wanandoa itadhaniwa kuwa ni mali inayomilikiwa na wanandoa wote kwa pamoja katika mafungu sawa. Dhana hii pia inaweza kukanushika.

- Mchango wa mume/mke katika ndoa unaweza kuwa wa hali na/au mali. Mfano ni Kesi ya Bi Hawa Mohamed iliyotambua mchango wa mama wa nyumbani katika kutunza na kupatikana kwa mali.
- Si ruhusa kwa mwanandoa kuweka rehani, kuuza, kutoa zawadi au kubadili umiliki binafsi wa mwanandoa mwenzake pasipo ridhaa yake. Pia mwanandoa hana ruhusa ya kumzuia mwanandoa mwenzake kumiliki mali au kugawa mali yake binafsi.

## Zawadi

Sheria inafafanua kuwa mali aliyopewa mwanandoa na mwanandoa mwenzake itahesabika kuwa mali ya yule aliyepewa. Dhana hii inaweza kukanushika.

## Madeni

Mwanandoa hatahusika na madeni ya mwanandoa mwenzake iwapo yamepatikana kabla ya kuwepo kwa ndoa. Madeni yatakayotokana na ununuzi wa mahitaji muhimu wakati wa ndoa yatalipwa na mume.

## Wanandoa na Sheria ya madhara (tort)

Aidha Sheria ya ndoa (kifungu cha 65) inaeleza kuwa mume hawezi kuwajibika kisheria kwa makosa ya daawa aliyotenda mke wake kwa sababu tu ni mume. Vilevile mwanandoa atawajibika kisheria kwa makosa ya daawa aliyomfanyia mwenzake bila kujali kuwa ni wanandoa. Hata hivyo mume au mke hana haki ya kufungua shauri la daawa kudai fidia kwa kosa linalotokana na uzembe au kushindwa kutimiza wajibu wa kuishi pamoja kama mume au mke.

## Ulinzi

Sheria ya Ndoa (Kifungu cha 66) inakataza mwanandoa kumdhuru mwanandoa mwenzake. Mfano vipigo kwa mwanandoa haviruhusiwi bila kujali mila za wanadoa hao.



## 1.10 Talaka na Kutengana

Sheria ya Ndoa, Sura Na. 29, kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 inatambua kuwepo mazingira yasiyoweza kurekebishika yanayoweza kupelekea ndoa kuvunjika, hivyo sheria huzungumzia talaka.

Talaka ni ruhusa ya kisheria ambayo mume au mke hupewa wakati anapomwacha mwenzie.

Chombo pekee chenye uwezo wa kuvunja ndoa ni MAHAKAMA. Kwa kawaida mahakama hutoa talaka kwa ndoa ambayo imedumu kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi. Lakini mahakama inaweza kutoa talaka hata kama ndoa haijadumu kwa kipindi hicho cha miaka miwili iwapo mlalamikaji atatoa sababu nzito sana.

## Kutengana

Kutengana sio talaka. Kutengana maana yake ni mume na mke kuishi mbalimbali. Kutengana kunaweza kuwa kwa mapatano kati ya mume na mke bila ya kufika mahakamani. Kuna aina mbili (2) za kutengana:

- Kutengana kwa mapatano
- Kutengana kwa amri ya Mahakama

## Sababu za kuomba au kutolewa Talaka

Zifuatazo ni sababu zinazoweza kupelekea kutolewa kwa talaka:

- Ugoni
- Ukatili
- Kulawiti
- Kichaa
- Uasi (Utoro)
- Kuzembea wajibu kwa makusudi
- Kifungo
- Dhana ya kifo
- Tofauti za itikadi au Dini
- Kutengana kwa wanandoa

## Utaratibu wa Kufuata wakati wa kuvunja ndoa

- Mwombaji atatakiwa kwenda Baraza la Usuluhishi la ndoa yaliyoteuliwa katika ngazi za wilaya kupitia ofisi za wlaya au katika taasis za dini zilizopewa kibali, Mfano: BAKWATA, Kanisani au Baraza la sheria la Kata.
- Mwombaji ataeleza shauri lake kwa Baraza husika na kama Baraza la Usuluhishi litashindwa kusuluhisha basi litatoa hati inayoruhusu shauri hilo lisikilizwe na Mahakama kwa utatuzi.
- Mwombaji ataandaa madai ya kuvunja ndoa na atayawasilisha Mahakamani kama utaratibu wa kisheria unavyoelekeza.
- Ukiambatanisha cheti cha ndoa kama kipo, hati ya Baraza la Usuluhishi na hati yoyote ile ambayo ungependa Mahakama ione.



## Viambatanisho muhimu wakati wa kuwasilisha madai ya Talaka

1. Cheti cha ndoa kuonyesha kwamba kulikuwa na ndoa halali
2. Ainisha sababu za kuwepo kwa mgogoro baina ya wanandoa mfano, ugoni, ukatili n.k na madhara yaliyotokea
3. Barua ya Baraza la usuluhishi kuthibitisha kuwa jitihada za kusuluhisha mgogoro zimeshindikana
4. Andaa hati ya madai ya talaka na kuonyesha
    - Ndoa ilifungwa lini, aina ya ndoa, muda wa ndoa, mahali mlipoishi
    - Taja watoto wa ndoa, jinsi na umri wao kama wapo
    - Taja mali mliyochuma wakati wa ndoa yenu
    - Omba mahakama mambo unayopenda yatolewe uamuzi kama:
        i. Ndoa imevunjika na talaka itolewe au kuwepo utengano wa muda kwa wanandoa
        ii. Mgawanyo wa mali mliyochuma
        iii. Mamlaka ya kukaa na watoto pamoja na matunzo yao iwapo unaona unahitaji na unaweza kukaa nao
        iv. Mwenzi wako alipe gharama za kesi
        v. Amri nyingine yoyote ambayo mahakama itaona inafaa



# SEHEMU YA 2

## SHERIA ZA MIRATHI TANZANIA

### 2.1 Utangulizi

Mirathi ni utaratibu mzima unaotumika katika kugawa mali ya marehemu pale anapofariki. Msimamizi wa mirathi ndiye mwenye jukumu kubwa la kuainisha mali iliyoachwa na marehemu, kutambua warithi halali, kugawa mali ya marehemu, kulipa madeni kama yapo na kuhakikisha mirathi inafungwa mara baada ya kukamilisha ugawaji.

Kutokana na mila, desturi, tamaduni na mazoea yaliyopitwa na wakati mara nyingi mjane hujikuta katika hali ya manyanyaso mara anapofiwa na mumewe. Mifano halisi imeshuhudiwa na taasisi zinazotoa huduma za kisheria kwa wanawake. Mifano hiyo ni pamoja na wajane kunyang'anywa mali na watoto, kufukuzwa katika nyumba, kunyimwa usimamizi wa mirathi, kutuhumiwa kuua waume zao kwa sababu mbalimbali na kulazimishwa kuolewa na ndugu wa marehemu.

### 2.2 Aina za Sheria za Mirathi Tanzania

Tanzania ina sheria tatu tofauti za mirathi ambazo ni:

1. Sheria ya Kimila ya Mirathi,Tangazo la Serikali Namba 358 la Mwaka 1963.
2. Sheria ya Mirathi ya Kiislamu.
3. Sheria ya Serikali ya Mirathi ya Mwaka 1865 [ Indian Succession Act 1865].

| **Muhimu** |
|---|
| Sheria hizi tatu (3) hutumika pale tu ambapo marehemu hakuacha wosia. Iwapo kuna wosia basi mali itagawanywa kwa kufuata wosia huo. Kwa muislamu hataweza kuhusia zaidi ya 1/3 ya mali yake. |

### Matumizi ya Sheria za Mirathi.

Sheria itakayotumika kugawa mali ya marehemu itategemea aina ya maisha aliyoishi marehemu wakati wa uhai wake kama ifuatavyo:

Marehemu aliyekuwa akiamini na kufuata dini ya kiislamu, mirathi yake itagawanywa kwa taratibu za dini ya kiislamu.

Marehemu aliyekuwa mtanzania asiye na asili ya kihindi au kisomali aliyeishi kulingana na mila na desturi za kabila lake sheria itakayofuatwa ni ile ya kimila (Sheria ya Kimila ya 1963 ni kwa makabila ya mkondo wa baba pekee).

Marehemu aliyeachana na mila na desturi za kabila lake na ambaye hakuwa muislamu basi Sheria ya Serikali 1865 itatumika kugawa mali yake.



## Sheria ya Kimila ya Mirathi

Msimamizi wa mirathi ni kaka mkubwa wa marehemu.

Warithi wa mali za marehemu ni watoto wake ambao wamegawanywa katika madaraja matatu (3):

- Daraja la kwanza- Mtoto wa kiume wa kwanza.
- Daraja la pili- Watoto wa kiume wote waliobaki.
- Daraja la tatu- Watoto wote wa kike.

**Mjane mwenye watoto:** Mjane hana fungu la urithi ila atarithi kupitia mgongoni kwa watoto na ataishi katika nyumba ya ndoa mpaka atakapoolewa au kufariki.

Mjane Mgumba: Sheria ya kimila inasema mjane mgumba atapata 1/20 ya mali iliyoachwa na marehemu.

| **Muhimu** |
|---|
| • Sheria hii inapingana na Katiba kwa kuwa inamnyanyasa mjane na watoto wa kike. Ni sheria inayohitaji kubadilishwa.<br>• Iwapo mjane ataweza kuthibitisha kuwa marehemu alikuwa ameachana na mila na desturi za kabila lake basi kuna uwezekano wa Sheria ya Serikali kutumika. |

Watoto wa nje ya ndoa hawatarithi ila kama tu wamehalalishwa kwa kufuata mila na desturi za kabila husika.

| **Mfano:** |
|---|
| • Kabila A: mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa atahalalishwa kwa kuchinja mbuzi na damu yake kupakwa katika sikio la mtoto huyo na baadaye kuingizwa katika nyumba ya familia.<br>• Kabila B: mtoto atahalalishwa kwa baba wa mtoto kutoa ng'ombe dume kwa familia ya mama wa mtoto.<br>• Kabila C: mtoto atahalalishwa kwa kutoa debe mbili za mtama, kiasi cha pesa kwa mama wa mtoto na nguo. |

## Sheria ya Mirathi ya Kiislamu.

Mjane/wajane kama kuna watoto atarithi/watarithi moja ya nane (1/8) ya mali ya marehemu.

Mjane/wajane kama hakuna watoto atarithi/robo (1/4) ya mali.

Watoto wa kike hupata fungu moja na mafungu mawili huenda kwa watoto wa kiume.

Mtoto wa nje ya ndoa kwa dini ya kiislamu hawezi kurithi.



## Sheria ya Kiserikali

Warithi walioainishwa katika sheria ya Serikali ni mjane/mgane na watoto.
Mjane atapata 1/3 ya mali na 2/3 iliyobaki kugawanywa sawa kwa watoto wote.
Mjane asiye na watoto atapata ½ ya mali ya marehemu na ½ iliyosalia itakwenda kwa wazazi wa marehemu.

## 2.3 Wosia

Wosia ni kauli au maandishi anayotoa mtu kuhusu namna mali yake angependa igawanywe iwapo atafariki. Wosia ulioandikwa kisheria unaweza kuepusha migogoro baina ya ndugu au jamaa kwani kauli au maandishi hayo ndio maamuzi ya mwisho katika kugawa mali ya marehemu.

| **Muhimu** |
|---|
| Mali inayomilikiwa binafsi au kwa pamoja na mwingine, ikiwemo ya ndoa inaweza kuandikiwa wosia. Kwa mali inayomilikiwa kwa pamoja na mwingine, mtoa wosia ataandika wosia wake kwenye mali hiyo kwa kiwango cha asilimia au hisa anayomiliki tu. |

| **Mfano:** |
|---|
| • Iwapo kuna nyumba moja ya ndoa, mwanandoa anaweza kutoa/kuandika wosia juu ya umiliki wa nyumba hiyo kwa asilimia ile aliyochangia.<br>• Iwapo kuna biashara ya pamoja na mwanandoa mwenzako, mwanandoa anaweza kutoa/kuandika wosia kwa kiwango cha asilimia/hisa/nguvu aliyowekeza katika biashara hiyo. |

## Aina mbili (2) za Wosia

Wosia wa mdomo
Wosia wa mdomo ni wosia unaotolewa kwa njia ya kauli na si maandishi. Wosia wa mdomo unapaswa kutolewa:

- Mbele ya mashahidi wasiopungua wanne. Wawili kati ya hao wanne wawe ndugu wa karibu na mtoa wosia na wengine wawili wanaweza kuwa watu baki.
- Na mtu asiyejua kusoma na kuandika, ingawa pale anapohitaji kutoa wosia wa maandishi sheria itaruhusu kuandikiwa.

## Mtoa wosia ni lazima:

- Awe mwenye akili timamu.
- Aliyetimiza umri uliokubalika kisheria, miaka 18.
- Mashahidi wote wanne wawepo kwa wakati mmoja.
- Mrithi hawezi kuwa shahidi wa mtoa wosia.



## Wosia wa maandishi

Wosia wa maandishi unapaswa kutolewa:

- Mbele ya mashahidi wasiopungua wawili.
- Kwa mwosia asiyejua kusoma mashahidi wasiopungua wanne.
- Uandikwe kwa kalamu ya wino na si risasi.
- Uwe na tarehe na sahihi ya mtoa wosia na kama mwosia hajui kusoma na kuandika ataweka sahihi kwa kidole gumba cha mkono wa kulia.
- Utaje jina la msimamizi wa mirathi.

| **Muhimu** |
|---|
| • Wosia ni siri hivyo ni muhimu kuteua mashahidi wanaoaminika na kuuhifadhi mahali salama.<br>• Wosia unaweza kubadilishwa na mtoa wosia kwa kukanusha wosia uliopita na kuandika mpya. Wosia mpya lazima uzingatie masharti ya uandikaji wosia. |

## 2.4 Utaratibu wa Kufungua Mirathi

### Iwapo Marehemu ameacha wosia:

1. Lazima kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya ambayo kifo kimetokea. Muda wa kisheria wa kuandikisha ni siku 30 tangu kifo kilipotokea.
2. Msimamizi aliyependekezwa na marehemu kwenye wosia ndiye mwenye mamlaka ya kufungua shauri la mirathi katika mahakama husika. Utaratibu wa kisheria unaelekeza kuwa mirathi zote za kimila au kiislam zitafunguliwa katika Mahakama ya Mwanzo wakati mirathi zitakazofuata taratibu za sheria ya serikali itafunguliwa Mahakama ya Wilaya au Mahakama Kuu ya Tanzania.
3. Iwapo wosia haukumtaja msimamizi wa mirathi basi mkutano wa ukoo ukae na kupendekeza mtu kuomba usimamizi huo.
4. Baada ya mahakama kupokea maombi ya usimamizi huo, itatoa utaratibu wa muombaji kugharamia tangazo la mirathi katika gazeti. Tangazo hilo litatoa muda wa siku 90 kuruhusu poingamizi toka kwa mtu yeyote anayepinga muombaji kupewa usimamizi wa mirathi.
5. Mahakama itatoa ruhusa kwa msimamizi wa mirathi aliyeteuliwa kugawa mali kwa kufuata wosia.

### Iwapo marehemu hakuacha wosia:

1. Lazima kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya ambayo kifo kimetokea. Muda wa kisheria wa kuandikisha ni siku 30 tangu kifo kilipotokea.
2. Mkutano wa ukoo ukae na kupendekeza jina au majina ya msimamizi wa mirathi.
3. Baada ya mahakama kupokea maombi ya usimamizi huo, itatoa utaratibu wa muombaji kugharamia tangazo la mirathi katika gazeti. Tangazo hilo litatoa muda wa siku 90 kuruhusu poingamizi toka kwa mtu yeyote anayepinga muombaji kupewa usimamizi wa mirathi.
4. Msimamizi atawajibika kugawa mali ya marehemu kwa warithi waliokubalika katika mahakama, na kwa kufuata sheria.



### Nakala au taarifa muhimu katika shauri la mirathi:

i. Nakala ya muhtasari wa kumbukumbu wa kikao cha ukoo
ii. Nakala ya wosia, iwapo marehemu aliacha wosia
iii. Majina ya warithi halali wa mali za marehemu
iv. Cheti cha kifo
v. Cheti cha ndoa, iwapo marehemu aliacha mke/mume
vi. Vyeti vya kuzaliwa vya watoto
vii. Taarifa muhimu za marehemu: majina, tarehe ya kufariki, jina la mwombaji, orodha ya mali alizoacha marehemu
viii. Nakala au taarifa zozote zitakazo hitajika mahakamani

## 2.5 Haki na Wajibu kisheria wa Msimamizi wa Mirathi

Msimamizi wa mirathi atakuwa na haki na wajibu kama ifuatavyo:

1. Kushitaki kuhusu suala lolote kama ambavyo angeweza kufanya marehemu kabla ya kifo chake.
2. Atatimiza wajibu wake sawa na kiapo chake alichowasilisha mahakamani.
3. Kukusanya madeni ya marehemu yaliyopatikana kabla au wakati wa kifo chake.
4. Kuhakikisha usalama, matunzo na usimamizi wa mali za marehemu.
5. Kugawa mali za marehemu kwa warithi waliobainishwa.
6. Kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia mazishi kwa kuzingatia hadhi ya marehemu aliyokuwa nayo, na utoshelevu wa mali zilizoachwa.
7. Kutoa taarifa mahakamani katika kipindi cha miezi 6 tangu kuteuliwa juu ya mali na madeni yaliyokusanywa, madeni ysliyolipwa na mgawo kwa warithi.
8. Katika kipindi cha mwaka 1 tangu uteuzi msimamizi aonyeshe mali zote zilizopita mikononi mwake na jinsi alivyozigawa.
9. Kutojinufaisha na mali za marehemu.

## 2.6 Mtitiriko katika kulipa madeni ya marehemu

Sheria ya urithi na usimamizi wa mirathi imebainisha jinsi ambavyo madeni ya marehemu yanatakiwa kulipwa kwa kutoa kipaumbele kama ifuatavyo:

i. Kwanza- Gharama za mazishi, gharama za matibabu.
ii. Pili- Gharama za ufunguzi na usimamizi wa shauri la mirathi zikiwemo gharama za kuendesha shauri hilo.
iii. Tatu- Malipo kwa huduma zilizotolewa kwa marehemu na mfanyakazi, kibarua au mtumishi wa nyumbani.
iv. Nne- Malipo kwa madeni mengine yaliyoachwa na marehemu.



## 2.7 Masuala Kumi (10) Umuhimu ya kujadiliwa kuhusu Mirathi:

1. Mkutano wa ukoo kutofanyika kutokana na wajumbe kutokuwa tayari kufanya hivyo kuzuia kupatikana kwa muhtasari ili kufungua mirathi.
2. Mjane kutopewa nafasi ya kuwa msimamizi au/na mrithi wa mali za marehemu mumewe na vitendo vingine vya udhalilishaji dhidi yake.
3. Kujitokeza kwa watoto wanaodai kuwa marehemu ni baba yao mara baada ya kifo chake wakati hawakufahamika hapo awali. Je mtoto uasiliwa kwa njia ipi?
4. Kutokuwa na taarifa au kumbukumbu sahihi juu ya mali za marehemu hasa pale ambapo alifanya biashara au shughuli za ubia na mtu au watu wengine. Ni kwa nini wanainchi wengi hawaandiki wosia?
5. Baada ya kifo kuzuka kwa mikataba aliyoingia marehemu na watu wengine juu ya mali zake hasa inayohusiana na madeni, mikopo, dhamana au uuzaji
6. Mchango wa mke katika ndoa kama jasho lake kuwekwa kama mali ya marehemu na kuwa sehemu ya mgawo katika urithi.
7. Mke anapofariki mirathi kutofunguliwa kwa kuwa mume bado yuko hai.
8. Msimamizi wa mirathi kuwa na nguvu juu ya mali katika kuzitumia kinyume na taratibu za sheria.
9. Je 'next of kin' au mtu wako wa karibu ina uhusiano wowote na taratibu za kisheria katika urithi au msimamizi wa mirathi?
10. Jamii inayoheshimu usawa na haki za binadamu kuendelea kutumia mila, desturi na tamaduni kama sababu za kuweka matabaka katika urithi kwa kutofautisha haki kwa makundi tofauti.



